Wanawake wenye Tumaini wa Finnish kwenye mbio kwa ajili ya kuchangia huduma

MSISITIZO: Kumsifu na Kumshukuru Baba Yetu-

Swahili

Matendo ya Bwana ni makuu! Yafikiriwa sana na wapendezwao nayo. Kazi yake ni heshima na adhama, Na haki yake yakaa milele. Amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu; Bwana ni mwenye fadhili na rehema! Zaburi 111:2–4.

Ni vyema kutafakari kuhusu maisha yetu,- kupata muda wa kukumbuka,- na kisha kusifu na kumshukuru Baba yetu kwa aliyoyatenda. Mtunga-zaburi kwenye mistari hapo juu anasema Mungu hutusababisha tukumbuke kazi zake za ajabu. Na majibu ya mtunga-zaburi ni nini? Anaanza kushukuru, akiimba; Jinsi Mungu wetu alivyo mwenye neema na rehema!

Unataka kumsifu Mungu kwa ajili ya nini? Kumbukumbu ipi inayokupa furaha na shukrani moyoni mwako unapokumbuka jinsi Mungu alivyoingilia kati na kukupa mahitaji yako? Ni uponyaji gani, faraja, upendo na uhuru ambao Mungu amekupa?

Lakini sifa zetu hazipo tu kutokana na baraka ambazo Mungu anatupa. Maisha mara nyingi yana vurugu na magumu pia. Unajikuta kwenye sehemu gani ngumu hata baada ya maombi, ukigundua kuwa Mungu anabaki kuwa na wewe na ndiye chanzo chako cha tumaini na amani katikati ya mapambano yanayoendelea?

Mwezi huu tunamsifu Mungu pia kwa kile anachofanya kwenye jamii yetu ya Wanawake wenye Tumaini wa TWR. Timu nyingi zinachukua hatua ya kufurahisha ya kuandika na kuandaa vipindi vyao wenyewe. Vikundi vya maombi vinawahudumia majirani zao, wafungwa na waliokamatwa na biashara ya binadamu. Mbegu ya Neno la Mungu imepandwa na inakua ndani ya mioyo ya wasikilizaji!

Na kwa hiyo, tunaungana na mtunga-zaburi kwa kupiga kelele za shangwe kwa Bwana. Tunamsifu na kumshukuru kwa sababu yeye ni Muumbaji wetu mzuri, ambaye ametuchukua kama watu wake na anatupenda kwa upendo wa milele!

Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote;
Mtumikieni Bwana kwa furaha; Njoni mbele zake kwa kuimba;
Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake;
Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake.
Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu;
Mshukuruni, lihimidini jina lake;
Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; Rehema zake ni za milele;
Na uaminifu wake vizazi na vizazi. (Zaburi 100)

twr WANAWAKE WENYE TUMAINI

TWR Wanawake wa Afrika wenye Tumaini • S.L.P 4232, Kempton Park, 1620, Afrika Kusini • +27 11 974 2886 • info@twrwomenofhopeafrica.org • twrwomenofhopeafrica.org

Baba, tunakusifu na kukushukuru ... Novemba 2019

1. …kwa mwanafunzi wa Asia ya Kati aliyewasiliana na timu ya Wanawake wenye Tumaini wa Norway. Akiwahimiza kuendelea kuwa waaminifu, kwa kuwa vipindi vyao vilikuwa tegemeo lake alipokuwa Mkristo pekee kijiji kwao	**2.** … kwa ongezeko la idadi ya wasikilizaji wa vipindi vya Wanawake wenye Tumaini kwenye ukurasa wa Facebook huko Romania. Timu inaweza kufikia watu wa rika tofauti, viwango vya elimu na madhehebu kwa njia hii.	**3.** … na tunachagua kulitangaza jina lako. Tunayafahamisha mataifa yale uliyoyafanya. Tunakuimbia sifa na kuwaambia watu ulimwenguni kote matendo yako ya ajabu. (Zab. 105: 1-2).
4. … kwa vipindi vya Wanawake wenye Tumaini nchini Tanzania vinarushwa kwa lugha ya Kiswahili kwenye vituo 10 vya FM. Baba, tunaomba watu wengi wakujue kama Mwokozi na kukua kwa kina kwenye uhusiano wao na wewe kupitia matangazo haya.	**5.** … kwa Timu ya Wanawake wenye Tumaini wa TWR watakaofanya maigizo kwenye Tamasha la Magereza la Romania mwezi Novemba. Tunaomba ukweli wa Mungu wa kiroho uwasilishwe vizuri kwa wafungwa na waweze kukuitikia.	**6.** … kwa mpango wa vipindi vya Wanawake wenye Tumaini wa Indonesia vinavyorushwa kwenye vituo 46 vya ndani na vipindi vya Javanisi kwenye vituo 22. Vipindi hivi vinafikia karibia Indonesia yote, vikiwapa wasioamini fursa ya kulisikia Neno la Mungu.
7. … kwa mbio kwa ajili ya huduma huko Finland zimeongeza fedha za Wanawake wenye Tumaini wa TWR nchini India. Timu ya Finland inashukuru kwa uhuru wa kuzungumza waziwazi kuhusu Yesu na kazi yao ya umishonari.	**8.** … kwa kutoa makazi mapya kwa wanawake waliouzwa nchini Albania. Pia, Wanawake wenye Tumaini wa TWR walishirikisha injili na vipindi vya Hazina zilizofichika kwa wanawake 8 waliosafari sh wa kibiashara waliokuja kwenye kambi yao.	**9.** … kwa injili kuendelea huko Ukraine. Tunakusifu kwa ajili ya dada zetu wanaotembelea nyumba za kulelea wagonjwa, hospitali na shule za bweni na kufundisha maadili ya Kikristo mashuleni. Neno lako liendelee kwa nguvu!
10. … kwa kumwadhimisha Yesu na kumkirimia jina lile lipitalo majina yote. Kwa jina la Yesu, kila goti lipigwe na ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba. (Flp. 2: 9-11).	**11.** … kwa wanawake wengi waliojiunga na kikundi cha maombi cha Serbia tangu mwezi Machi 2019. Mungu anahimiza mioyo yao wanapohudumiana kwa maombi na wanawake walio kwenye hali ngumu duniani.	**12.** …kwa watu wengi wanaojitolea barani i Afrika kushirikiana na timu za Wanawake wenye tumaini wa TWR. Kwenye mikutano yao, wao huungana na wengine wanaposhirikiana na kumimina mioyo yao.
13. …kwa namna vikundi vya maombi vya Wanawake wenye tumaini wa TWR vinavyohudumu na kuwafundisha wafungwa. Baba, fanya kazi yenye nguvu ya kusafisha na kurejesha maisha ya kweli kwa wanawake hawa na wanaume	**14.** … kwa wanaume na wanawake unaowalea kuwa mashujaa wa maombi wa Wanawake wenye Tumaini wa TWR nchini Ufaransa. Baba, walete waumini wengi zaidi kuungana nao, na uwafanye waaminifu kuutafuta uso wako.	**15.** … kwa kuwa unafanya kazi kwenye vijiji nchini Malawi na kufungua milango ya huduma. Tunakusifu kwa mchungaji anayekutana kuomba na wanawake 200 na pia anawahudumia wajane.
16. … kuwa wewe ndiye muanzilishi wa maisha. Tunashukuru kwamba baada ya miaka mitano ya kukataliwa, Sikukuu ya Maisha na Maandamano yalifanyika Septemba 14, 2019, Zurich, Uswizi.	**17.** … kwa kuwa kama vile tulivyompokea Kristo Yesu kuwa Bwana, tunatakiwa tuendelee kuishi ndani yake, tukisimikwa na kujengwa ndani yake, tukiimarishwa katika imani na kufurika kwa shukrani.(Wakol. 2:6-7)	**18.** … kwamba vipindi vya Wanawake wenye tumaini vinatangazwa kwa lugha ya Kitamil na ujumbe wake unawaelimisha wanawake, unawapa stadi kwa vitendo na hata kuwabariki wanaume wanaosikiliza.
19. … kwamba ahadi zilizo kwenye Neno lako ni za kweli na amina. Bwana, unaona shida za kila mtu. Na wanapokuita, unaingilia kwa wakati wako na kwa njia yako.	**20.** … kuwa Hazina zilizofichika inaandaliwa kwa lugha ya Kikorea. Tunaomba iweze kutumika kuwahudumia wanawake wa Korea Kaskazini ambao ni wakimbizi nchini China.	**21.** … kwa waombaji waliopo Kanada wanaoinua mahitaji ya maombi ya Wanawake wenye tumaini wa TWR kila siku. Tunawashukuru pia kwa wanaojitolea kwa uaminifu kuandaa barua kila mwezi.
22. … kwamba huko Uswizi vipindi vipya kwenye mgahawa wa Hanna vinaandaliwa na wanawake waliokata tamaa wanabadilishwa kuwa wanawake wenye ujasiri na matumaini.	**23.** … kwa wasikilizaji wa vipindi vya Wanawake wenye Tumaini wa Ureno. Wanawasiliana na Timu ya Waandaaji kufikisha ujumbe kuwa ni kwa ni kiasi gani vipindi vinabariki maisha yao.	**24.** … kwa kuwa tumechaguliwa, ni watakatifu na wasio na hatia mbele za Mungu. Tumekombolewa na kusamehewa na neema ya Kristo. Tumetiwa muhuri na Roho Mtakatifu. (Efe. 1: 4-13)
25. … kwa kuwa Wanawake wa Tumaini wa TWR nchini Ethiopia wataadhimisha miaka 10 ya huduma mnamo Januari 2019. Baba, endelea kuiongoza na kutoa mahitaji ya huduma hii.	**26.** … kwamba tunapaswa kufurahi siku zote, kuomba bila kukoma na kushukuru kwa kila jambo; kwa maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu. (1 Thes. 5: 16-18).	**27.** … kwa kutuma waandaji wa vipindi wenye vipaji wa timu ya Asia ya Kaskazini wanaoandaa vipindi vya Wanawake wenye Tumaini kwa lugha za Kivietinamu na Kijapani.
28. …kwa ajili ya vikundi vidogo na mashirika ambayo yako tayari kugawa Makala ya sauti ya hazina zilizofichika kwenye Wilaya hatarishi nchini Ujerumani.	**29.** …kwa ajili ya miaka 60 ya ushirika wenza kati ya TWR na ERF ya Ujerumani na kwa ajili ya ushirikiano wa ERF na wanawake wenye Tumaini wa TWR tangu mwanzo wa wahuduma ya TWR.	**30.** …kwa kuwa hatutakiwi kusumbukia kitu cha kula au kunywa au kuvaa kwa kuwa Baba wa mbinguni anajua mahitaji hayo yote. (Math. 6:31-32)